TAARIFA FUPI YA KUTEMBELEA SHUGHULI ZA VIJANA ZA KUCHAKATA ASALI KATIKA KITUO CHA VIJANA KALOVYA KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA NDUGU AMOUR HAMAD AMOUR TAREHE 04/04/2017

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,

Mradi huu wa kituo cha uchakataji wa asali ni moja ya jitihada za Halmashauri katika kuboresha sekta ya Maliasili hususani shughuli za ufugaji wa nyuki kwa kushirikisha vijana wajasiliamali. Mradi ulianza kutekelezwa mwaka 2015 kwa kushirikisha vijana wajasiliamali hasa wafugaji nyuki watakao kuwa wanakusanya na kufanya shughuli za uchakataji wa asali katika kituo hiki.

Mradi huu unahusisha jumla ya wanachama 28 wanaonufaika na mradi moja kwa moja ambao wanaume ni **25** na wanawake ni **3**. Tangu kuanzishwa kwa shughuli hizi wanachama wamenufaika kwa kupewa mafunzo ndani na nje ya Mkoa ikiwa ni pamoja na kupata ujuzi wa uchakataji kupitia vifaa vilivyopo chini ya usimamizi wa watalaam wa Halmashauri. Maendeleo ya shughuli hizi ni mazuri kutokana na ushirikiano wa wanachama wote, watalam kutoka Mradi wa Miombo na Jumuia ya wafugaji wa nyuki Inyonga ambao ni wadau wakubwa wa shughuli za nyuki.

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,

Malengo ya mradi huu ni kuleta chachu ya uzalishaji kwa njia ya kisasa wa mazao yatokanayo na nyuki na pia vijana hawa kua chachu ya mabadiliko katika sekta ya ufugaji nyuki kutoka ufugaji nyuki wa kienyeji kwenda ufugaji nyuki wa kisasa katika Halmashauri yetu, ikiwa ni pamoja na kuwaunganisha wafugaji wa nyuki na wafanyabiashara wa mazao ya Nyuki, kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao yatokanayo na nyuki, kupanua wigo wa masoko ndani na nje ya Halmashauri hatimaye kuongeza kipato na kuwaletea maisha bora wananchi wa Halmashauri hii.

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,

Kituo hiki kina uwezo wa kupokea na kuhifadhi tani 40 za Asali na Nta tani 10, kwenye chumba cha kuhifadhia asali, na pia kuna chumba cha kupimia ubora wa asali kwa kutumia kifaa kiitwacho **fractomita**, pamoja na chumba cha kuhifadhia vifaa, bomba la moshi (**bee smokers**), Kofia Maalumu ya Kujikinga wakati wa kulina Asali (**Straw hat**), Vazi maalumu la Kuvunia Asali (**protective suit**), kinga ya mikono (**Gloves**), kinga ya miguu (**gun boot**), Vifaa

vya mzinga (**Hive tool**), Chujio (**Strainer**), Mswaki wa kutolea nyuki kwenye masega (**Bee brush**), Vifungashio (**parking tools**) na Nembo (**Labels**).

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,

Kwa sasa Serikali ya Wilaya kwa kushirikiana na Mradi wa Miombi wako katika hatua za mwisho za ununuzi wa mtambo utakatotumika kuchaka asali na nta, kugredi na kufungasha katika viwango vya hali ya juu. Mtambo huu utagharimu kiasi cha **sh. 153,000,000.00** umeagizwa nje ya nchi na unatazamiwa kufika nchini mwishoni mwa Mwezi April, 2017 ambao vijana wa kituo hiki watautumia kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao yatokanayo na nyuki.

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,

Shughuli hizi za kupokea, kuchakata na kuhifadhi asali zinahusisha vifaa vyote vya uchakataji na ufungashaji wa mazao ya nyuki. Gharama za mradi huu ni shilingi 75,015,000.00 zinazohusisha gharama za ujenzi wa kituo cha vijana shilingi 71,000,000.00 zilizotolewa na Halmashauri na kiasi cha shilingi 4,015,000.00 zikiwa ni gharama za ununuzi wa vifaa vya kuanzisha na kuendesha shughuli hizi, fedha zilizotolewa namradi wa miombo unalojihusisha na utunzaji wa misitu na mazingira.

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,

Kwa heshima na taadhima tunaomba utembelee shughuli hizi za kukusanya, kuchakata na kuhifadhi mazao ya nyuki zinazofanywa na vijana katika kituo hiki.

Mwenge wa Uhuru 2017 Oyeeeeeeeeeeeeeeeee!!!!!!!!!!!!!!!!!!!

MRADI WA VIJANA KATIKA KITUO CHA KUCHAKAT ASALI INYONGA

TAARIFA FUPI YA KUTEMBELEA MOJA YA MRADI ULIYOTEMBELEWA NA MWENGE WA UHURU 2017 KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE KWA NDUGU CHARLES FRANCIS KABEHO KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA TAREHE 03/05/2018

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa uhuru kitaifa,

Mradi huu wa kituo cha kukusanya, kuchakata na kuuza mazao yatokanayo na nyuki (Asali na nta) Inyonga ni moja kati ya miradi na shughuli nyingine za kijamii zilizotembelewa na Mwenge wa Uhuru 2017 katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlele. Kituo hiki kilibuniwa na kuanza kutekelezwa na Halmashauri katika mwaka wa fedha 2014/15 na umeendelea kuboreshwa hadi sasa ambapo Mwenge wa uhuru umefanya matukio yafuatayo: 2015, jiwe la msingi, 2016 jiwe la ufunguzi wa kituo na Mwaka 2017 kutembelea shughuli kikundi cha vijana wasimamizi wa kituo wanaojishughulisha na kukusanya, kuchakata na kuhifadhi na kuuza mazao ya nyuki. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Halmashauri kwa kushirikiana na Mradi wa Miombo ilifanikiwa kupata mtambo wa kisasa wenye uwezo wa kuchakata na kufungasha tani 40 za asali kwa muda wa masaa 24 katika ubora wa hali ya juu, mtambo ambao umefungwa na sasa uko tayari kutumika.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa uhuru kitaifa,

Katika mwaka huu wa fedha 2017/18 Halmashauri imeendelea na ukamilishaji wa mifumo ya umeme na maji na kuwezesha umeme na maji kuingizwa kwani vyote vinahitajika katika kuendesha mtambo huu shughuli nyingine za ofisi na uendeshaji wa kituo hiki ambacho pia ni ofisi za SACCOSS ya vijana inayisimamiwa na Halmashauri ijulikanayo kama Inyonga Vijana SACCOSS.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa uhuru kitaifa,

Malengo ya mradi huu ni kuleta chachu ya uzalishaji kwa njia ya kisasa wa mazao yatokanayo na nyuki na pia vijana hawa kua chachu ya mabadiliko katika sekta ya ufugaji nyuki kutoka ufugaji nyuki wa kienyeji kwenda ufugaji nyuki wa kisasa katika Halmashauri yetu, ikiwa ni pamoja na kuwaunganisha wafugaji wa nyuki na wafanyabiashara wa mazao ya Nyuki, kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao yatokanayo na nyuki, kupanua wigo wa masoko ndani na nje ya Halmashauri hatimaye kuongeza kipato na kuwaletea maisha bora wananchi wa Halmashauri hii.

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,

Kituo hiki kina uwezo wa kupokea na kuhifadhi tani 40 za Asali na Nta tani 10, kwenye chumba cha kuhifadhia asali, na pia kuna chumba cha kupimia ubora wa asali kwa kutumia kifaa kiitwacho **fractomita**, pamoja na chumba cha kuhifadhia vifaa, bomba la moshi (**bee smokers**), Kofia Maalumu ya Kujikinga wakati wa kurina Asali (**Straw hat**), Vazi maalumu la Kuvunia Asali (**protective suit**), kinga ya mikono (**Gloves**), kinga ya miguu (**gun boot**), Vifaa

vya mzinga (**Hive tool**), Chujio (**Strainer**), Mswaki wa kutolea nyuki kwenye masega (**Bee brush**), Vifungashio (**parking tools**) na Nembo (**Labels**).

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa uhuru Kitaifa,

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,
Gharama za mradi huu zimefikia sh.……ambazo zimetokana na vyanzo vifuatavyo: sh.71,000,000 zilitolewa na Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa kituo, uwekaji wa mfumo wa umeme na maji, kiasi cha sh. 4,105,000 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya uvunaji wa asali na uchakataji na sh. 159,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa mtambo wa kuchakata na kufungasha asali zilizotolewa na mradi wa Miombo

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,
Katika Mbio za Mwenge wa Uhuru, 2017 Mwenge wa Uhuru ulizindua na kufungua miradi nane (8), uliweka mawe ya msingi katika miradi miwili (2), alitoa misaada ya kiutu na mikopo kwa vikundi vinne (4) na kufungua klabu 2 mbili (2). Gharama za miradi yote, misaada, klabu na mikopo ilyotolewa ilikuwa shilingi 2,040,086,091.00, ambapo shilingi 254,668,140.00 zilichangwa na wananchi, shilingi 412,624,222.00 zilitoka Halmashauri, shilingi 1,056,890,230.00 zilitoka Serikali Kuu na shilingi 33,033,500.00 zilitoka kwa wahisani. Miradi iliyozinduliwa na kufunguliwa inaendelea vizuri na inatumika kama ilivyopkusudiwa, na miradi miwili iliyowekewa mawe ya msingi yote ikiwa ni miradi ya kimkakati ya viwanda vidogo inayojumuisha ujenzi wa ghala la kuhifadhi mazao pamoja na ufungaji wa mashine za kubangua karanga imekamilika kwa asilimia 80 na yote inatumika, kilichobaki ni upanuzi wa miradi hii kulingana na mpango.

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,
Orodha ya miradi yote na shughuli za kijamii zilizotembelewa na Mwenge wa uhuru 2017 zimeambatishwa katika jedwali ambalo pia linatoa taarifa za kila mradi

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa,
Kwa heshima na taadhima, tunaomba utembelee kituo hiki cha kuchakata asali ambao ni miongoni mwa miradi iliyotembelewa na Mwenge wa uhuru 2017 na utuzindulie mtambo huu ili uanze kutumika rasmi

HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE

TAARIFA YA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTEMBELEWA KATIKA MBIO ZA MWENGE WA UHURU

TAREHE 04/04/2017

Na	Jina la Mradi	Sekta	Shughuli iliyofanyika	Gharama za mradi	Hali halisi kufikia Machi, 2018	Picha ya Mradi
1	Klabu ya vijana ya kuendeleza michezo na kupambana na dawa za kulevya kata ya Utende	Michezo/ Afya	Kuzindua klabu	1,200,000	Klabu zinaendelea vizuri, klabu zinatembelewa kila robo ya mwaka	
2	Shamba la miti lenye ukubwa wa ekari 9 la wakulima wa tumbaku kijiji cha Mtakuja	Maliasili	Uzinduzi wa shamba	25,472,272	Shamba linaendelea vizuri linahudumiwa na kuongezwa. Hadi kufikia Machi, 2018 ekari…..za shamba limeongezwa na kupandwa jumla ya miti……	
3	Ujenzi wa nyumba ya walimu yenye uezo wa kuwezesha walimu 6 kuishi pamoja shule ya sekondari Ilela	Elimu Sekondari	Ufunguzi	161,466,400	Nyumba, inatunzwa na inatumika kama ilivyokusudiwa na imepunguza idadi ya walimu wasio nyumba katika shule ya sekondari ilela kutoka……hadi…….	
4	Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa shule ya sekondari Ilela	Elimu Sekondari	Ufunguzi	90,860,000	Madarasa yalikamilika na yanatumika. Mradi umepunguza upungufu wa	

					vyumba vya madarasa katika shule hii kutoka.....hadi.....	
5	Vyandarua 100 kwa ajili ya wanafunzi 50 wa bweni na akina mama wajawazito 50 shule ya sekodari Ilela/kijiji cha Ipwaga	Afya	Kugawa msaada wa vyandarua	1,000,000	Vyandarua vilitolewa na elimu inaendelea kutolewa kwa makundi mbalimbali juu ya matumizi sahihi ya vyandarua	
6	Nyumba 5 za wakuu wa idara wa Halmashauri	Utawala	Ufunguzi	239,036,250	Nyumba zinatumika. Kwa sasa Halmashauri iko katika mipango ya kuingiza maji na umeme ili kuboresha mradi baada ya umeme kuwashwa katika mji wa inyonga mwaka huu wa fedha 2017/18. Ulazaji wa bomba za maji umeanza.	
7	Kutembelea shughuli za vijana wanaojishughulisha na mradi wa uchakataji asali kijiji cha Kalovya	Nyuki	Kutembelea/kukagua shughuli za vijana ka	83,924,416	Baada ya kutembelewa na Mwenge wa uhuru 2017, mradi umeendelezwa kwa kuwekewa umeme, kununua na kufunga mtambo wa kuchakata asali	
8	Ujuenzi wa barabara ya lami yenye urefu wa kilomita 2.84 katika mji wa Inyonga	Barabara	Kufunguliwa	1,004,908,808	Barabara imekamilika na inatumika	
9	Ujenzi wa nyumba ya kulala wageni Inyonga (Lusambo Annex)	Sekta binafsi	Kufunguliwa	180,000,000	Mradi ulikamilika na umekuwa msaada mkubwa kwa wageni wa kiserikali, wafanyabiashara n. k	
10	Ujenzi wa ghala la mazao la mfanyabiashara kijiji cha Inyonga	Kilimo	Jiwe la msingi	70,000,000	Umaliziaji, kwa sasa mradi unaendelea kupanuliwa na kuwa kiwanda kidogo cha kubangua karanga ambapo	

					mashine ….zimefungwa na zinatumika	
11	Kutembelea shughuli za karakana ya vijana Inyonga	M/Jamii		0.00	Vikundi vya vijana vinaendelea na shughuli, na kwa mwaka huu, wanaisaidia Halmashauri katika kutengeneza milango katika mradi wa mwenge	
12	Uzinduzi wa mfumo wa maji safi na maji taka Hospitali tarajiwa ya Wilaya	Maji	Ufunguzi	116,691,416	Mradi ulikamilika na unatumika. Kwa sasa mradi umeendelezwa na maji yamepelekwa stendi mpya ya mabasi Inyonga. Huduma za upasuaji ziliwezeshwa mara baada ya mradi huu.	
13	Ukarabati wa wodi kwa ajili ya kupata chumba cha upasuaji hospitali tarajiwa ya Wilaya	Afya	Uzinduzi wa huduma	27,000,000	Mradi ulikamilika na huduma inatolewa kwa ufanisi mkubwa kama ilivyokusudiwa. Huduma zilianza kutolewa mwezi…., 2017 na hadi Machi 2018 jumla ya wagonjwa waliopasuliwa ni…..na hakuna vifo….	
14	Msaada wa baiskleli 18 kwa wenyeviti wa vijiji 18	Mipango/ Utawala	Kukabidhi msaada	3,050,000	Baskleli zilikabidhiwa na utendaji wa wenyeviti wa vijiji umeonesha kuboreka	
15	Mkopo wa mashine ya kukamua mafuta ya karanga kwa kikundi cha akinamama Lekatugeme wa kijiji cha Masigo	M/Jamii	Kukabidhi mkopo	7,420,000	Ujenzi wa jengo la kusimika mashine	
16	Klabu ya kupambana na kuzuwia Rushwa ya watendaji wa vijiji	Sheria/Utawala	Kuzindua klabu	856,000	Klabu inaendelea, mafunzo yanaendelea kutolewa na wanaklabu wamepewa baiskeli kwa ajili ya	
17	Vifaa vya shule kwa	M/Jamii	Kukabid	1,200,000	Watoto walikabidhiwa msaada	

	wanafunzi yatima (Shati, sketi, kaptula,viatu, soksi, begi, daftari na kalamu)		hi msaada		na Halmashauri inaendelea kuwafuatilia	
18	Kiwanda kidogo cha kubangua karanga cha mfanyabiashara katika mji wa Inyonga	Viwanda/ Sekta binafsi	Jiwe la msingi	35,000,528.20		
	Jumla			**2,049,086,091.00**		

Na	Miradi liyoziduliwa/Funguliwa	Mawe ya Msingi	Misaada ya kiutu na mikopo
1	8	2	4